# MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILIOCHO FANYIKA KATIKA OFISI YA KITENGO MANUNUZI TAREHE 25/10/2021

**WALIOHUDHURIA.**

| | |
|---|---|
| 1. DR CAINAN KISWAGA | MWENYEKITI |
| 2. HAMAD MFINANGA | -KATIBU |
| 3. ADDINANI. MWENDA | -MJUMBE |
| 4. FREDERICK .E. MMBAGA | -MJUMBE |
| 5. UPENDO KIVUYO | -Mwalikwa |

**PMU:**

| | |
|---|---|
| 1. FLORIAN CHRISTIAN | -SECRETARIAT |
| 2. ERICK LIWOLA | -SECRETARIAT |

**WASIOHUDHURIA.**

| | |
|---|---|
| 1.ROSE .P. MAHIKU | -Kwaatarifa |

**AGENDA.**

1. KUFUNGUA KIKAO.
2. KUTHIBITISHA MUHTASRI WA KIKAO CHA TAREHE 23/07/2021
3. ONGEZEKO LA MPANGO WA MANUNUZI WA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 . KUTOKA TSH. **5,029,960,012.92** HADI TSH. **6,828,777,152.00**
4. OMBI LA UNUNUZI KWA NJIA YA FORCE ACCONT KWA MIRADI YA AFYA NA ELIMU YENYE JUMLA YA SHILINGI. **1,798,817,140.00**
5. TAARIFA YA MANUNUZI ROBO YA KWANZA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.
6. KUFUNGA KIKAO

## AGENDA NAMBA 1. KUFUNGUA KIKAO.

Mwenyekiti alifungua kikao saa 8:00 mchana kwa kuwakaribisha wajumbe walio hudhuria kikao hicho.

## AGENDA NAMBA 2. KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 23/07/2021

Katibu alisoma Muhutasari wa kikao cha bodi ya zabuni kilichofanyika tarehe 23/07/2021 na baada ya wajumbe kujadili Muhtasari tajwa hapo juu wajumbe waliridhia kuwa muhtasari huo kuwa kumbukumbu halali za kikao cha bodi ya zabuni.

**AGENDA NAMBA 3. ONGEZEKO LA MPANGO WA MANUNUZI WA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 . KUTOKA TSH. 5,029,960,012.92 HADI TSH.6,828,777,152.00**

**Katibu aliwasilisha ombi la ongezeko la mpango wa manunuzi wa mwaka 2021/2022 kutoka Tsh.5,029,960,012.92 hadi kufika Tsh.6,828,777,152.00. na alieleza hii nikutoka na kupata fedha za miradi ya afya na elimu , yenye jumla ya Tsh.1,798,817,140.00 na mchanganua wake nikama ifuatavyo**

**MCHANGANUO FEDHA HIZO ZILIZOONGEZEKA KWA MIRADI YA ELIMU NA AFYA**

| S/N | JINA LA MRADI | CHANZO CHA FEDHA | KIASI KILICHOTOLEWA |
|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa Madarasa 56 katika shule sekondari | GAVI | 1,120,000,000/= |
| 2 | Ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum | GAVI | 80,000,000.00 |
| 3 | Umaliziaji wa madarasa04 madarasa03 yunta na kirangare 01 | SERIKALI KUU | 50,000,000.00 |
| 4 | Ujenzi wa vituo vya afya vya Tarafa | SERIKALI KUU | 500,000,000.00 |
| 5 | Ujenzi wa mifumo yakunawia mikono,uvunaji wa maji,uwekaji wa maji ya bomba uchimbaji wa visima shule za msingi kishaa,jiungeni na sekondari ndungu | GAVI | 35,617,139.58 |
| 6 | Ujenzi wa matundu ya vyoo katika shule za msingi za Chanika na Jiungeni | EP4R | 13,200,000.00 |
| | JUMLA KUU | | **1,798,817,140.00** |

Baada yakatibu kuwasilisha ombi hilo wajumbe walijadili na waliridhia badiliko hilo la mpango wa manunuzi wa mwaka wa fedha 2021/2022 kuwa Tshs. 6,828,777,152.00.

**AGENDA NAMBA. 4 OMBI LA UNUNUZI KWA NJIA YA FORCE ACCONT KWA MIRADI YA AFYA NA ELIMU YENYE JUMLA YA SHILINGI. 1,798,817,140.00**

Katibu aliwasilisha maombi yakufanya manunuzi kwa njia ya force akaunti(force account) kwenye miradi ya vituo vya afya tarafa na miradi ya elimu madarasa 56 shule za sekondari ,ujenzi wa bweni lawanafunzi maalum,umaliziaji madarasa vunta na kirangare,ujenzi wa mifumo ya kunawia mikono shule za kishaa,jiungeni na ndungu sekondari.
Wajumbe walijadili ombi hilo la manunuzi kwanjia ya force akaunti na kuridhia manunuzi haya yafanyika kwanjia ya force akaunti kwenye miradi ya elimu na afya yenye jumla Tsh. 1,798,817,140.00

**AGENDA NAMBA. 5. TAARIFA YA MANUNUZI ROBO YA KWANZA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.( JULY, AGOSTI NA SEPTEMBER 2021)**

**Katibu alisoma taarifa ya Manunuzi kwa kipindi cha robo ya kwanza 2021/2022 ambayo ilionyesha kwamba vifaa pamoja na huduma mbalimbali zilizotolewa kwa Halmashauri ziligharimu jumla ya shilingi.199,476,103.71. Aidha katibu alifafanua kuwa manunuzi kwakipindi cha robo kwanza yalifanyika kwanjia ya LPO ngazi ya wilaya yaligharimu shilingi 58,957,280/=, manunuzi yaliyofanyika katika zahanati na vituo vya afya na hospitali yaligharimu shilingi 31,626,802/=, manunuzi yaliyofanyika katika shule za sekondari yaligharimu shilingi 78,621,477.71/=, manunuzi yaliyofanyika katika shule za msingi yaligharimu shilingi 30,270,544/= baada ya ufafanuzi huo wajumbe walijadili taarifa hiyo walipokea na kukubali kuwa kumbukumbu halali zakikao cha bodi ya zabuni.**

**AGENDA NAMBA. 6. KUFUNGA KIKAO**

**Mwenyekiti alifunga kikao saa 10.30 jioni kwa kuwashukurub wajumbe kwamichango na mawazo waliyotoa katika kufanikisha kikao hicho**

..........................................

Dr. Cainan Kiswaga

MWENYEKITI

..........................................

Hamad Mfinanga

KATIBU